



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



## UWEKAJI WAZI DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Mikoa ya Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora, Katavi, Kigoma, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Njombe na Songwe kuwa itaweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa **siku saba (7)** kuanzia tarehe 01 hadi 7/05/2025, katika vituo vyote viliviyotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura.

1. **SIKU:** Uwekaji wazi wa daftari la awali la wapiga kura utafanyika tarehe 1-7 Mei, 2025
2. **VITUO:** Uwekaji wazi wa daftari Awamu ya Pili utafanyika katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika.
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

### Utaratibu wa kuhakiki.

Mpiga kura anaweza kuhakiki taarifa zake kwa njia zifuatazo:-

1. Mpiga Kura mwenyewe kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho.
2. Kupitia simu yake ya kiganjani kwa kupiga namba \*152\*00# na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
3. Mpiga kura kupiga simu namba 0800112100 na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
4. Mpiga Kura kuhakiki taarifa zake kupitia Tovuti ya Tume, [www.inec.go.tz](http://www.inec.go.tz) kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa ‘uhakiki’ na kuendelea kufuata maelekezo.

### Mambo ya kuzingatia.

1. Iwapo mpiga kura amehakiki taarifa zake kwa kutumia njia yoyote kati ya hizo nne na kutaka kufanya marekebisho ya taarifa zake atatakiwa kwenda Kata husika na kufanya marekebisho hayo.
2. Mpiga Kura anayehitaji kumuwekea pingamizi Mpiga Kura asiye na sifa za kuwemo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ataenda katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika.
3. Mtu mmoja katika familia anaweza kukagua na kuhakiki taarifa za majina ya familia nzima.

Limetolewa leo tarehe 17 Aprili, 2025 na

Kaimosi, K. K.  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**